

# Malipo ya Kidijitali

## Usimamizi wa Biashara na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika wa Kidijitali kwa Wanawake Wajasiriamali Wadogo

*Ripoti hii imeweza kufanikishwa kwa ushirikiano wa ukarimu na watu wa Marekani kupitia Uwakala wa Marekani wa Maendeleo ya Kimataifa (USAID). Muongozo huu ulitolewa chini ya Mradi wa Frontia za Kidijitali za DAI (Cooperative Agreement AID-OAA-A-17-00033) kutokana na ombi la USAID wakishirikiana na Mastercard.*

# Taaswira ya Moduli

## Jedwali la yaliyomo


**Sehemu ya 1:** Thamani ya kujishughulisha kidijitali kwa wanawake kwenye biashara 5

**Sehemu ya 2:** Utangulizi wa pochi za simu 9

**Sehemu ya 3:** Utangulizi wa malipo ya kidijitali 18

**Sehemu ya 4:** Yanayofaa kufanywa na kutofanywa kwenye malipo ya kidijitali 29


## Malengo

1. Jifunze jinsi ya kukubali malipo ya kidijitali kwenye duka lako.
2. Elewa faida za malipo ya kidijitali.

## Kwenye Moduli hii, unaweza…

- kufanya mazoezi ya kufungua pochi ya simu na akaunti ya merchant
- jifunze jinsi ya ku-skani kodi ya QR
- jadili faida za malipo ya kidijitali


Kabla hujaanza, hebu tuone ufahamu wako wa teknolojia ya malipo ya kidijitali!
Wangapi kati yenu mnaokubali malipo ya kidijitali kwenye maduka yenu?
Wangapi kati yenu mnaokubali malipo ya kidijitali kwenye maduka yenu?
Wangapi kati yenu wanaomiliki na kutumia pochi ya simu?

# SEHEMU YA 1:
# THAMANI YA KUJIHUSISHA KIDIJITALI KWA WANAWAKE KWENYE BIASHARA

**Malengo:** Ili kuelewa thamani na faida ya wanawake kutumia vifaa vya kidijitali katika biashara.





## Utumiaji wa teknolojia haujalenga kutumiwa na jinsia maalum.

Ufanisi na ujuzi unatokana na mazoezi na nafasi.

Kila mtu  anaweza kujifunza jinsi ya kutumia teknolojia. Ni kufanya mazoezi tu!


# Kwanini unahitajika kuwa na Pochi yako ya Simu

1 **Unapata uhuru mwingi wa kujitegemea.**
Ukiwa na pochi yako ya simu, utaweza kudhibiti wakati na jinsi ya kutumia pesa.

2 **Unakuwa muelewa sana kwenye teknolojia ya kidijitali.**
Mazoezi yanakufanya mkamilifu! Utakuwa na ufahamu zaidi kwenye vifaa vya kidijitali na teknolojia ikiwa utakuwa na pochi yako ya simu.

3 **Shughulika kwa ufanisi na salama.**
Ukiwa na pochi ya simu, huhitaji kutumia muda wako kusafiri na kusubiri benki. Unakuwa umebeba shughuli zako salama na kwa siri kwenye simu yako, nyumbani, au kwenye biashara.

4 **Inajukumu kubwa kwenye fedha za duka lako.**
Ukiwa na udhibiti wa pochi yako ya simu, unaamua jinsi unavyotaka kuitumia kwenye duka lako. Unaweza pia kutumia shughuli za data kukusaidia kufanya maamuzi kuhusu duka lako, kama vile bidhaa gani za kununua kulingana na rekodi zao za mauzo.




Sofía na mume wake Mateo wote wanafanya kazi dukani. Licha ya kuwa Mateo ndiye mmiliki mkuu, Sofía ana uwezo sawa wa kufanya maamuzi na kuchangia kwenye usimamiaji uendeshaji na fedha dukani. Mateo ana furaha kuwa na Sofía wakifanya kazi pamoja dukani. Anatoa mawazo yakusaidia na hata kumfunza baadhi ya mambo. Hakuwa anaweza kuendesha duka peke yake bila yeye!

# SEHEMU YA 2: UTANGULIZI WA POCHI ZA SIMU

**Malengo:**

1. Kujifunza kuwa pochi ya simu ni nini, na ni kwanini na jinsi ya kuitumia.
2. Kuelewa jinsi ya kuseti pochi ya simu, na maelezo yanayohitajika ili kufungua moja.



# Pochi za Simu ni nini?



**Pochi ya simu ni pochi ya kweli inayokaa kwenye simu yako. Unaweza kutumia pochi yako ya simu kwa mambo mengi, kama vile kutuma pesa, kupokea malipo kutoka kwa wateja, kulipa bili za huduma zako, kununulia vitu dukani, kununua bidhaa za duka lako na zaidi!**

Pochi za simu ni aina ya huduma ya fedha ya kidijitali – haihusishi pesa taslimu.

Pochi za simu zinaweza kuwa na majina tofauti. Zinaweza kuitwa "pochi za kidijitali," "Pochi za kielektroniki," au "mfuko wa kidijitali." Na orodha inaendelea!

# Aina ya Watoa Huduma wa Pochi ya Simu



Pochi za simu zinatolewa na watoa huduma mbalimbali. Watoa huduma tofauti wanaweza kuita pochi zao za simu majina tofauti. Nchi moja inaweza kuwa na watoa huduma wengi wa pochi ya simu, au idadi ndogo.

**Kampuni za Simu.** Nchi nyingi, kampuni za simu zinatoa "huduma za mobile money" inayowaruhusu watumiaji kutuma, kuweka, na kupokea pesa kwa kutumia simu zao. Utahitajika kufungua akaunti ya mobile money au pochi ya simu, lakini akaunti ya benki haihitajiki. Unahitaji tu simu ya kawaida! Wakati mwingine unaweza pia kutumia akaunti yako ya mobile money kuhamisha pesa hadi kwenye akaunti yako ya benki, ikiwa unayo.

**Benki.** Benki zinaweza kutoa huduma za benki za simu, zinazoruhusu watumiaji kutumia simu zao kusimamia akaunti zao za benki. Baadhi ya nchi, benki pia zinatoa huduma za mobile money pale ambapo kumiliki akaunti ya benki hakuhitajiki.

**Fintech (Teknolojia ya Kifedha).** Kampuni nyingi za fintech, ufupisho wa "teknolojia ya kifedha," hutengeneza programu na huduma ambazo zinawaruhusu watumiaji kutekeleza shughuli za kifedha. Wakati mwingine wanafanya kazi na akaunt ya benki, lakini sio kila mara utahitaji akaunt ya benki ili kuzitumia.

# Faida za Pochi za Simu

**Pochi za simu mara nyingi ni rahisi kutumia kuliko pochi za kawaida.** Zinaweza kuokoa wakati kwa kukuruhusu wewe kupokea na kulipa malipo ya hopo kwa hapo, hata kutoka kwa wateja ambao hawapo dukani kwako. Huhitaji kwenda benki kuweka mapato yako; badala yake, unaweza kufanya shughuli hizo kwa siri ukiwa kwako nyumbani na dukani! Pia hutakuwa na wasiwasi wa kubeba pesa taslimu ili kuzivunja au kuwalipa wasambazaji wako.

**Pochi za simu zinaweza kukulinda.** Pale ambapo pochi yako ya kawaida inaweza kuibiwa, pochi yako ya simu imeweka nywila za usalama zinazopunguza hatari ya kuibwa.

**Pochi za simu zina matumizi mengi.** Unaweza kuzitumia kulipa wasambazaji wako, kuchangia akiba zako na shirika la mkopo au akaunti ya akiba, kulipa bili, kutuma pesa kwa marafiki na familia, kupokea pesa kutoka kwa wateja, kununua nafaka, kulipia nauli, na zaidi! Pia watoa huduma wanakuja na matumizi zaidi kila wakati. Matumizi yanaendelea kuwa mengi!



# Kuwalipa Wasambazaji



Hujambo Imani! Mambo yanaendeleaje kwenye duka lako?

Sijambo Sofía! Duka linaendelea vizuri, huwa tunakuwa bize sana wakati huu wa mwaka.


Ni vizuri kusikia hivyo! Kwa kweli nina tatizo kidogo kwenye duka langu. Nina oda ya orodha ndefu mwisho wa juma hili, na nina wasiwasi kuhusu kuweka pesa zote hizo dukani ili kuwalipa wasambazaji.

Oh! Ahaa! Umeshazingatia kuwalipa wasambazaji wako kwa pochi yako ya simu? Ni haraka na rahisi kutumia! Na pia, huhitaji kuwa na wasiwasi kuhusu kuwa na pesa taslimu.


Waw! Sikujua unaweza kufanya hivyo kwa kutumia pochi yako ya simu.

Huoni ni njia bora? Nalipia mazao yangu na wasambazaji wa vinywaji kwa kutumia pochi ya simu. Na pia huweka oda mapema kwa wasambazaji wangu ili walete kwa wakati.

Ahsante sana Imani, Nitajaribu kutumia njia wasambazaji wakija!



# Ada ya shughuli za Pochi ya Simu




**Baadhi ya shughuli za pochi ya simu ni bure, kama vile kuweka pesa kwenye pochi yako. Kuangalia salio huwa bure pia! Hata hivyo, sio shughuli zote za pochi ya simu ni bure. Kwa kawaida utahitajika kulipa ada wakati unatoa pesa kielektroniki na kuzibadilisha kuwa pesa taslimu. Na pia ni kawaida kulipa ada ya shughuli wakati unatuma pesa kwa mtu mwengine.**

Ni muhimu kuangalia ada zinazohusika na pochi yako ya simu! Unaweza kuangalia wavuti wa mtoaji huduma wako au kwenda kwa wakala kuangalia ada za pochi yako ya simu. Wakala ni mtu ambaye anafanya kazi kwa niaba ya kampuni ya simu, benki, au fintech kutekeleza shughuli za pochi ya simu. Wakati mwingine, unaweza kupata ilani au arafa ikikuonyesha ada kwenye pochi yako ya simu.

# Jinsi ya kuseti Pochi ya Simu

**Kumbuka: Watoaji huduma wanaweza kuhitaji maelezo tofauti na kuwa na hatua tofauti za kufungua pochi ya simu.**

1

**Kwanza,** chagua mtoa huduma wako wa pochi ya simu.

2

**Pili,** pakua programu ya mtoa huduma au tembelea wavuti wao, na chagua hatua ya kuanza usajili. Ikiwa una simu yenye vipengele, utahitajika kutembelea wakala ili kufanikisha mchakato wa usajili.

3


**Jaza sehemu zinazohitajika.** Kawaida, utahitajika kuandika jina lako, anwani, na kutoa ithibati ya utambulisho, kama vile kitambulisho chako au kitambulisho cha kadi ya uraia, leseni ya udereva, au pasipoti.

4

**Kingine,** tengeneza kodi ya PIN yako au nywila yako. PIN yako au nywila ndio jinsi utafikia pochi yako ya simu. Ni muhimu kuweka nambari kuwa siri.

**Sasa utakuwa umejisajili** na unaweza kuanza kutumia pochi yako ya simu kutuma na kupokea pesa!



**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

# Pochi ya Simu na Hey Sister





## Masomo ya Hey Sister

**Somo la 2: Naseti vipi akaunti ya mobile money?**


Sasa tujadili!
Kuna yeyote mwenye mpango wa kufungua pochi yao ya simu baada ya kipindi hiki?
Ni faida zipi zingine unazoweza kufikiria za kuwa na pochi yako ya simu?
Utatumia vipi pochi yako ya simu kwenye biashara yako?

# SEHEMU YA 3:
# UTANGULIZI WA MALIPO YA KIDIJITALI




**Malengo:**

1. Kujifunza kuhusu malipo ya kidijitali na faida zake.
2. Kuelewa jinsi ya kutumia malipo ya kidijitali kwenye biashara.

# Anzisha Teknolojia kwenye duka lako




- Wezesha malipo ya kidijitali
- Pata ID ya merchant na kodi QR ili kuwezesha wateja kukulipa haraka na kwa urahisi
- Kuwa na mashini mahali pa kuuzia (POS) ili kuboresha usimamizi dukani na bidhaa na kupata data ili kufuatilia biashara yako inavyokua
- Chukua oda kwa njia ya simu, Arafa, au WhatsApp



# Malipo ya kidijitali ni yapi?



**Malipo ya kidijitali ni shughuli inayofanyika kupitia mtandaoni au njia za “kidijitali”, kama vile kupitia simu yako au kifaa kilichounganishwa kwenye mtandao wa simu.**

Malipo ya kidijitali yanajulikana pia kama malipo yasiyotumia pesa taslimu, kwa kuwa hakuna pesa taslimu zinazohusishwa.

Mfumo wa malipo ya kidijitali unatumia teknolojia kufanikisha mauzo na ununuzi badala ya pesa taslimu.

Baadhi ya huduma za malipo ya kidijitali ni: POS, Kodi ya QR, pochi ya malipo, na USSD.

# Faida za Malipo ya Kidijitali

- Kushughulika kwa urahisi
- Kuwa na rekodi ya mkopo na kuboresha uwezo wa kupata mkopo kutoka kwa idara rasmi
- Kusimamia akaunti zako bila matatizo
- Kuweka akiba ya pesa
- Kushughulika kwenye hatari ya kiwango cha chini kuliko kulipa kwa kutumia pesa taslimu
- Kuwa na udhibiti imara kwenye mapato yako
- Kukusanya malipo kutoka kwa wateja na wasambazaji wakiwa mbali
- Kupata ziada ya pesa taslimu au kupewa pointi
- Kupata utambuzi wa kina wa pesa zinavyoingia na kutoka, namna unavyotumia, na usimamizi wa pesa



# Kulipa Bili Kidijitali




Imani, Siku hizi nimekuwa nikitumia muda mwingi sana dukani kwa kulipa bili zangu! Inanichukua saa nyingi kulipa bili zangu zote na kupata pesa za kutosha. Unajua njia yoyote rahisi ya kulipa bili?

Umewahi kujaribu kulipa bili zako kidijitali? Huwa nalipa bili zangu mtandaoni au kupitia pochi yangu ya simu.

Waw! Nafikiria nitaanza pia kulipa bili kidijitali. Nitaenda kupendekeza kwa mume wangu, Mateo!

Pia nitaseti malipo ya bili kioto kupitia pochi yangu ya simu ili kamwe nisije kuacha malipo! Inanisaidia kujipanga vizuri, na sasa nalipa vizuri bili zangu kwa wakati kila mwezi.




# Uelewaji wa Malipo ya Kidijitali

**Malipo ya kidijitali sio salama na ni hatari.**

**Malipo ya kidijitali yana ugumu wa kuseti na kuyamudu.**

**Malipo ya kidijitali ni ghali.**




**Malipo ya kidijitali yanaweza kuwa salama kuliko kulipa kwa pesa taslimu.** Kwa kawaida unahitajika kuthibitisha malipo yako ya kidijitali kwa PIN au neno la siri. Pia, serikali huchapisha masharti yanayohitaji mtoaji huduma ya pochi ya simu kuweka pesa zako salama.

**Pindi utakapojua jinsi ya kufanya, malipo ya kidijitali ni rahisi kutumia** na yanaweza kufanikishwa kwa kubonyeza vitufe kadhaa.

**Gharama ya malipo ya kidijitali yanaweza kutofautiana.** Wakati mwengine kunaweza kuwa na ada, baadhi ya shughuli huwa bure. Unaweza pia kuokoa muda wa kulipa bili na kuweza kufikia wateja zaidi.


Sasa tujadili!
Ni maswali gani unayo kuhusiana na malipo ya kidijitali?
Kuna mtu yeyote anayetaka kuseti malipo ya kidijitali kwa biashara yake?
Unaweza kufikiria faida zingine zozote za malipo ya kidijitali?

# Jinsi ya Kuseti Akaunti ya Merchant ya Biashara Yako




**1**

Tembelea wavuti wa mtoaji huduma wako au tembelea wakala kuanza usajili.

**2**

Jaza maelezo yanayohitajika, kama vile jina lako, nambari ya usajili ya biashara, anwani ya baruapepe, anwani, na ID (Kitambulisho).

**3**


Baada ya kujisajili, inaweza kuchukua muda maombi yako kukubaliwa.

**4**

Ni hivyo tu! Ukishakubaliwa, utapata nambari ya merchant ID na kodi ya QR ili wateja waweze kukulipa.

# Kutaka Kujua Kodi ya QR

- “Kodi ya QR” inamaanisha “Quick Response Code” ni aina ya bakodi ya 2D ambayo inasomwa na simu za kisasa.
- Kodi za QR zinawezesha kuhamisha pesa kwa haraka na rahisi kati ya akaunti.
- Kodi za QR zinatumia teknolojia salama kwa kuhamishia pesa.
- Hakuna maelezo ya benki yanayohitajika kujaza ili kutumia kodi ya QR.
- Kadi za kawaida hazihitaji kutumia kodi ya QR.



**Teknolojia rahisi kutumia ya malipo ya kidijitali**

Baada ya kutengeneza kodi yako ya kipekee ya QR, ichapishe na uining’inize kwenye sehemu ya kulipia ya duka lako.

# Jinsi ya kulipa kwa kutumia kodi ya QR




1. Fungua Programu ya kamera yako
2. Skani kodi ya QR
3. Thibitisha mchakato wa malipo
4. Ni hivyo tu! Malipo yako yalifanywa baada ya sekunde chache

**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

# Malipo ya kidijitali na Hey Sister




## Masomo ya Hey Sister

**Somo la 5: Naseti vipi akaunti ya merchant ya biashara yangu?**
**Somo la 24: Ni vipi alama iliyowekwa ya kidijitali inaweza kutoa nafasi kwa biashara yangu?**

# SEHEMU YA 4: YANAYOFAA NA YASIYOFAA KWENYE MALIPO YA KIDIJITALI

**Malengo:** Kujifunza vidokezo na ujanja wa kulinda maelezo yako ya mtandaoni.



# Yanayofaa kwenye Malipo ya Kidijitali

- Pakua programu halisi na zilizo rasmi.
- Seti nywila imara ya kutumia kuingia kwenye programu zako na akaunti.
- Uwe ukiangalia salio kwenye akaunti yako na rekodi za shughuli zako.
- Badilisha nywila yako mara kwa mara.
- Funga simu yako kila wakati ili kuzuia matumizi yasiyoruhusiwa.
- Toka kwenye programu zako na akaunti wakati huzitumii.



# Yasiyofaa kwenye Malipo ya Kidijitali

Usiache simu yako kama huitumii huku ukiwa umeingia kwenye programu za benki kwenye simu.

Usitumie nywila moja kwenye programu zako zote na akaunti.

Usihifadhi nywila yako ya shughuli za benki kwenye simu. Ikariri au uiandike mahali na uifiche mahali salama.

Usionyeshe mtu yeyote nywila, PIN, au maelezo mengine ya siri.

Usitumie mitandao wa Wi-Fi isiyo salama.



# Sheria na Masharti



**Watoaji huduma ya Malipo ya kidijitali huwa wanatoa "Sheria na Masharti" kwenye wavuti zao, ambayo yamebeba maelezo muhimu kuhusiana na simu yako au pochi ya kidijitali.**

Yanaweza kuwa yamebeba maelezo kuhusu unachohitajika kufanya na nani wa kuwasiliana naye wakati simu yako, PIN, au kadi ya SIM imepotea au kuibwa.

Ni muhimu kuangalia sheria na masharti ya mtoaji huduma wako ili kuona njia zote ambazo unaweza kulindwa wakati unatumia malipo ya kidijitali.

**NYENZO YA KUFUNDISHIA**

# Jifunze Kuhusu Haki Zako na Hey Sister




**Masomo ya Hey Sister**

**Somo la 12: Haki zangu ni zipi kwa mujibu wa sheria na masharti ya mobile money?**

# Mambo Makuu ya Kuzingatiwa kutoka kwa Hii Moduli



1. **Pochi za simu na akaunti za merchant zinakupa uthibiti imara wa fedha zako.** Kufungua pochi yako mwenyewe ya simu au akaunti ya merchant ya biashara yako itakupa wewe uhuru mwngi wakifedha. Unaweza kuamua ni wapi utatenga pesa zako, na vile utatumia pochi zako za kidijitali.
2. **Malipo ya kidijitali yanatoa nafasi nzuri, siri, na inayopatikana.** Ukiwa na malipo ya kidijitali, pochi za simu, na akaunti za merchant, hutahitaji tena kusafiri kwenda kwenye benki yako na kusubiri kwenye foleni ili kufanya shughuli zako. Ukiwa na vifaa hivyo, unaweza kutoa na kuweka pesa salama na kwa siri ukiwa mahali popote, ikiwemo dukani kwako au nyumbani kwako.
3. **Kwa kutumia vifaa vya kidijitali kunakupa rekodi za kuingia na kutoka kwa pesa.** Kutumia malipo ya kidijitali kutakupa mtiririko wa kidijitali wa shughuli zako, unaoweza kukusaidia wewe kufanya muhimu kuhusu biashara yako, kama vile ni bidhaa gani za kununua.
4. **Vifaa vya kidijitali vinaweza kuifanya biashara yako kuwa na ufanisi sana vikitumiwa vyema.** Ni muhimu kuchukua tahadhari wakati unatumia pochi za simu na kukubali malipo ya kidijitali. Kumbuka kukagua shughuli zako mara kwa mara, matumizi ya nywila kwenye vifaa vyako, na kujizuia kuonyesha maelezo ya siri na mtu yeyote.




Tuma mashaka yako na maswali!

USAID

KUTOKA KWA WATU WA MAREKANI

STRATEGIC IMPACT ADVISORS



[www.siaedge.com](http://www.siaedge.com)

Laini ya Pili

Laini ya Tatu

